NJIA 60 ZINAZOTUMIWA NA UMOJA WA MATAIFA KULETA MABADILIKO

Kitabu kimetafsiriwa na

BI. Mary Naimeri Kubo – Nairobi

Mhazili – Mwazighe Mshila – Chuo Kikuu cha Kenyatta.

MAADHIMISHO YA SITINI YA KUANZISHWA KWA UMOJA WA MATAIFA NI WAKATI UFAAO WA KUTAFAKARI YOTE AMBAYO SHIRIKA HILI IMEFANYA KWA MUDA MREFU. LIMEKUWA MSTARI WA MBELE KUTEKELEZA MENGI KATIKA KIPINDI CHA MWISHO CHA KARNE YA ISHIRINI NA KATIKA MWANZO WA KARNE YA ISHIRINI NA MOJA HUKU LIKIZUIA MAANGAMIZI YA VITA, KUONGEZA MUDA WA KUISHI, KUWASAIDIA WATU WALIOKUMBWA NA MAAFA, KUHIFADHI MALI YA ASILI NA MAZINGIRA NA KUSIMAMIA HAKI ZA BINADAMU ULIMWENGUNI. SHIRIKA HILI PIA LINASHUGHULIKA KUKUZA UTANDAWAZI NA KUONA KWAMBA UMASKINI UMEANGAMIZWA NA USIWE TENA HALI HALISI YA MAISHA.

MAADHIMISHO HAYA YA SITINI YANATUKUMBUSHA KWAMABA DUNIA LEO NI TOFAUTI NA ILE YA WAANZILISHI WAKE. UMOJA WA MATAIFA LAZIMA UTAFAKARI MWANZO HUU MPYA NA KUKABILIANA NA CHANGA MOTO ZIFUATAZO: KWANZA KABISA NI UTAMBUZI KWAMBA WATU WENGI WANGALI WANAATHIRIWA NA NJAA, MAGONJWA NA MAZINGIRA YASIYOFAA ILHALI ULIMWENGU UNA UWEZO WA KUWAOKOA. UMOJA WA MATAIFA ULIO NA ARI NA NGUVU MPYA LAZIMA USAIDIE KULETA MABADILIKO NA KUFANYA KAZI WENZI WINGI ILI KUFANIKISHA MAADILI YA WAANZILISHI.

KOFI ANNAN
24 OKTOBA 2005

Umoja wa Mataifa ulianzishwa baada ya vita vilivyofanya uharibifu ili kuleta utulivu kati ya mataifa ulimwenguni na kuimarisha misingi ya amani.

Kati ya tishio la vita vya kitonoradi na migororo na nchi isiyoisha, uimarishaji wa amani umekuwa swala muhimu la Umoja Wa Mataifa na hasa kwa jeshi lake la amani la askari wanaovaa kofia za rangi ya bluu.

Lakini Umoja Wa Mataifa ni zaidi ya chombo cha kuimarisha amani na Baraza la kusuluhisha migororo. Umoja wa Mataifa na jamii ya mawakala wake hushughulika kufanya kazi ya kujaribu kuinua hadhi ya maisha ya watu wanaoishi ulimwenguni bila ya kujitangaza.

Ustawi na kuishi kwa watoto. Uhifadhi wa Mazingira. Haki za Binadamu. Afya na Utafiti wa Tiba. Upunguzaji wa Umaskini na Maendeleo ya Uchumi. Ustawi wa Kilimo na Uvuaji. Elimu. Maendeleo kwa wanawake. Msaada wa dharura katika maafa. Usafiri wa pangani na baharini. Matumizi ya amani ya nguvu za kiharamu. Haki za kazi na wafanyikazi. Orodha inaendelea.

Kwa muhtasari tu ni baadhi ya shughuli zilizotimizwa na Umoja Wa Mataifa na mawakala wake tangu kuanzishwa kwa ushirika huo mwaka wa 1945.

1 KUKUZA MAENDELEO

Umoja Wa Mataifa umejitolea kwa hali na mali ili kustawisha maisha ya watu, vipawa na ujuzi kote ulimwenguni. *Tangu mwaka wa 2000, kazi hii imeelekezwa na Ustawi wa Mikakati ya MileniaMillenium Development Goals [MDGs]*. Mfumo wa Umoja Wa Mataifa wa gharama ya matumizi ya Ustawi baada ya kuondoa Taasisi za Kifedha Ulimwenguni ni dola bilioni $10. kwa mfano Shirika la Umoja Wa Mataifa la mipango na maendeleo *UNDP* lililo na wafanyikazi katika shughuli za UN za kumaliza Umaskini na kustawisha utawala mzuri katika nchi zinazoendelea ulimwenguni. Shirika la Umoja Wa Mataifa la Hazina ya watoto *UNICEF* linafanya kazi katika nchi 157 na hutuma kiasi cha fedha zaidi ya dola bilioni $1.2 kwa mwaka kwa kulinda watoto, kuwapa chanjo, kukabiliana na UKIMWI na kutoa elimu kwa wasichana. Shirika la Umoja Wa Mataifa la mikutano ya Biashara maendeleo UNCTAD husaidia nchi kwa kutoa nafasi za kuendeleza biashara zao. Zaidi ya hayo, Benki ya Dunia hutoa mikopo kwa nchi zinazoendelea za jumla ya dola bilioni $18 hadi bilioni $20 kwa mwaka na imesaidia miradi ya kimaendeleo zaidi ya 9,500 tangu mwaka wa 1957. Fedha zote zinazotumiwa kwa missada kwa maendeleo hutoka kwa michango inayotolewa na nchi mbalimbali.

2. KUKUZA DEMOKRASIA

UN imesaidia kukuza na kuimarisha Taasisi za kidemokrasia kote Ulimwenguni. Imesaidia watu kutoka nchi nyingi kuweza kushiriki katika uchaguzi na haki na uhuru, nchi kama Cambodia, Namibia, El Salvodor, Eritrea, Mozambique, Nicaragua, Afrika Kusini, Kosovo na Timor Mashariki. Imetoa ushauri na usaidizi katika uchaguzi pamoja na usimamizi ya matokeo kwa zaidi ya nchi 90 hasa wakati maalum katika historia kama nchi za Afghanistan, Iraq na Burundi.

3. KUKUZA HAKI ZA BINADAMU

Tangu Baraza kuu lilipokubali. Haki za Binadamu Ulimwenguni miaka 1948, Umoja Wa Mataifa umesaidia kufanya mikataba ya haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kuwa sheria shirika la UN la Haki za binadamu limefanya uchunguzi wa malalamiko ya kibinafsi ya kesi ya mateso ulimwenguni, Kupotea na kuwekwa kizuizini bila sababu na kufaulu kuhimiza serikali ulimenguni kuimarisha na kuboresha rekodi zao za Haki za kibinadamu.

4. KUDUMISHA AMANI NA USALAMA

Kwa kutuma idadi ya wanajeshi 60 kudumisha amani pamoja na mashirika ya kushuhudiashughuli hizo katika sehemu zilizokumbwa na shida Ulimwenguni; Mwaka huu wa 2005, Umoja Wa Mataifa umeweza kuleta amani kwa otoshlevu ili kuwezesha majadiliano kuendelea na kuokoa mamilioni ya watu wasiwe wahasiriwa wa vita. Kwa sasa kuna nyendo za vikosi vya jeshi vya kuweka amani 17 kote ulimwenguni.

5. KULETA AMANI

Tangu mwaka wa 1945, UN imesaidia katika majadaliano ya kuleta amani kwa zaidi ya vikao 170 vya amani ambavyo vimechangia kumaliza migororo ya nchi mbalimbali. Mifano ni kama kumaliza vita kali ya Iran na Iraq, kuchangia katika kuondoka kwa wanajeshi wa Urusi kutoka Afghanistan na kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini El Salvador na Guatemala. Umoja Wa Mataifa umetumia diplomasia ya utuliu ili kuepuka vita.

6. KUHIFADHI MAZINGIRA

Umoja Wa Mataifa unashughlika kutatua shida za mazingira Ulimwengu. UN kama Baraza la Ulimwengu la kujadiliana na kuleta makubaliano kuhusu shida kama mabadiliko ya hali ya anga umalizaji wa tabaka ozoni, taka za za sumu, kuangamia kwa misitu na uharibifu wa hewa na maji. Shida hizi zisipotatuliwa masoko na njia za uchumi hazitaweza kuhimiliwa kwa muda mrefu kwani uharibifu wa mazingira unaangamiza sehemu ya asili ambapo uhai wa binadamu unategemea.

7. KUZUIA UENEAJI WA SILAHA ZA NYUKLIA

Kupitis kwa shirika la Umoja Wa Mataifa la Nishati za Atomiki (IAEA) husaidia kuona kwamba nchi zinazotumia teknolojia za nyuklia haziundi silaha za aina hiyo kwa siri. Mamia ya maeneo yaliyo na nyuklia husimamiwa na IAEA katika zaidi ya nchi 70. hivi sasa kuna mikataba 237 iliyokubaliwa katika nchi 152 ya kulinda makubaliano hayo.

8. KUKUZA NA UHURU

UN ilipoanzishwa mwaka wa 1945, watu milioni 750 yaani zaidi ya thuluthi moja ya idadi ya watu ulimwenguni waliishi katika serikali zilizotegemea zile za kikoloni. Umoja Wa Mataifa ulichangia katika kuleta uhuru kwa zaidi ya nchi 80 ambazo ni mataifa huru.

9. KUHUKUMU WAHALIFU WA VITA

Mahakama zilizoanzishwa na UN katika nchi za Yugoslavia na Rwanda zimehukumu wahalifu wa vita na kuwafunga gerezani, kuanzisha sheria muhimu ya kesi zinazohusu uangamizaji wa kabila au taifa na haki za binadamu na kasha kutoa kiwango cha haki ambayo imekubaliwa kama jambo muhimu na watu wan chi iliyoathiriwa.

10. KUMALIZA UBAGUZI WA RANGI AFRIKA KUSINI

Umoja Wa Mataifa ulifaulu na kuchangia katika kuangamiza mfumo wa Ubaguzi wa rangi kwa kutumia mbinu kama kuzuia silaha na hata kupinga ubaguzi katika michezo. Uchaguzi uliofanyika Afrika kusini mwaka wa 1994 uliruhusu watu wake wote kushiriki kikamilifu bila ubaguzi na ukawa mwanzo wa serikali ya jamii nyingi.

<<<<<<<<<<<<<<<” TUNASIMAMA HAPA LEO KUSHUKRUR USHIRIKA WA UMOJA WA MATAIFA NA MATAIFA WANACHAMA, SHUKRANI ZAO BINAFSI NA PAMOJA KWA KUUNGANA NA WANANCHI KWA LENGO MOJA LA KULETA UKOMBOZI NA KUSUKUMA MYUMA MISINGI YA UBAGUZI WA RANGI.

RAIS NELSON MANDELA wakati wa hotuba yake kwa Baraza kuu la Umoja Wa Mataifa 1994, mwaka ambao uchaguzi wa kwanza kufanywa nchini Afrika kusini na kushirikisha watu wa rangi zote.

11. KUIMARISHA SHERIA ZA ULIMWENGU

Zaidi ya mikataba mingi juu ya haki za binadamu, ugaidi, uhalifu ulimwenguni, wakimbizi, upunguzaji wa silaha, bidhaa na bahari zimepitishwa kuwa sheria kwa sababu ya juhudi ya Umoja wa Mataifa.

12. KUTOA MISAADA YA FADHILA KWA WAKIMBIZI

Zaidi ya wakimbizi milioni hamsini wanaokimbia vita, njaa au mateso wamewahi kupata misaada kutoka kwa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Balozi anayeshughulika wakimbizi (UNHCR) tangu mwaka wa 1951 kama hatua ya kuendeleza juhudi za mawakala wengine. Shirika hili linazua mbinu za kudumu za kuwasaidia wakimbizi wanaorudi makwao ikiwa hali itaruhusu au kuwasaidia ili waweze kuhamia katika nchi yao mpya au kuhama katika nchi ya tatu. Kuna zaidi ya wakimbizi milioni 19 wanaotaka vibali vya kuhamia nchi nyingine na wale waliomo nchi mwao lakini hawana makao hasa wanawake na watoto ambao hupata chakula, makao, matibabu, elimu na usaidizi wa kuwarudisha makwao kutoka kwa UN.

13. KUMALIZA NJAA YA MARA KWA MARA NA UMASKINI MASHAMBANI KATIKA NCHI ZINAZOENDELEA

Hazina ya Kimataifa kwa maendeleo ya kilimo (IFAD) imeanzisha mfumo wa kutoa mikopo mara kwa mara ikiwa ya kiwango kidogo ili iwasaidie watu maskini kutoka mashambani waangamize umaskini. Tangu kuanzishwa kwa mfumo huu, IFAD imetumia fedha zaidi ya dola bilioni $8.5 kugharama miradi na mipango 676 iliyowanufaisha watu zaidi ya 250 milioni. Fedha za IFAD zinatoka kwa michango kibinafsi kutoka kwa nchi mbalimbali.

14. KUTOA MSAADA KWA WAKIMBIZI WAPALESTINA

Ijapokuwa jumuia ya ulimwengu inajibidisha ili kuona kwamba amani ya kudumu kati ya Wapalestina na Waisraeli imepatikana, Wakala/Ajenti ya Umoja wa Mataifa ya kazi kwa wakimbizi wa Palestina Mashariki ya karibu UNRWA imekuwa ikiwasaidia vizazi vine vya wakimbizi wa kipalestina kwa kuwapa elimu, matibabu, huduma za jamii, mikopo midogo ya fedha na misaada ya dharura. Zaidi ya wakimbizi milioni 4 katika mashariki ya kati wamejisajili na Ajenti hii ya UNRWA.

15. KULENGA USTAWI WA KIAFRIKA

Bara la Afrika inaendelea kupewa kipaumbele na Umoja wa Mataifa. Mwaka wa 1986, UN iliandaa mkutano maalum ili kuipigia debe Afrika ipate kuungwa mkono na nchi za ulimwengu na kusaidia kufufua uchumi na maendeleo. Mwaka wa 2001, viongozi wan chi za Kiafrika waliukubali mkataba wa Bara lao,Ukia mpya kwa Ustawi wa Afrika (NEPAD) ambao ulikubaliwa rasmi na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka wa 2002 kama mfumo wa kuelekeza misaada kwa Bara la Afrika. Bara hili hupata asilimia 33% ya mifumo wa UN wa matumizi kwa ustawi zaidi ya mataifa mengine. Mashirika yote ya UN yana mipango maalaum kwa manufaa ya Afrika.

16. KUKUZA HALI NJEMA YA WANAWAKE

Umoja wa Mataifa umesaidia kukuza usawa na hali njema ya afya kwa wanawake. Shirika la Umoja wa mataifa la ustawi kwa wanawake (UNIFEM) na lile la utafiti na taasisi za mafunzo kwa ustawi wa wanawke ulimwenguni (INSTRAW) yamesaidia kuinua hali ya maisha kwa wanawake na kukuza haki za wanawake kwa zaidi ya nchi 100. INSTRAW hufanya utafiti na kutoa shughuli za mafunzo ilhali UNIFEM ikisaidia miradi inayonuia kuangamiza vurugu dhidi ya wanawake, kuleta mageuzi na kubadilisha uenezaji wa UKIMWI na kukuza ualama wa kiuchumi kwa wanawake. Kwa mfano, kwa kungeza nafasi za kazi na haki ya kuweza kurithi ardhi. Mashirika yote ya UN yanafaa kushughulika mahitaji ya wanawake.

17. KUKUZA HAKI ZA WANAWAKE

Lengo kuu la Umoja wa Mataifa la muda mrefu limekuwa ni kuboresha maisha ya wanawake na kuwapa mamlaka ya kudhibiti maisha yao. Mwaka wa 1975 UN iliandaa mkutano wa kwanza wa wanawake nchini mexico na pamoja na mikutano mingine ilidhaminiwa na UN, Ajenda ya wanawake katika karne ulimwenguni ya kuendeleza haki zao ilibuliwa. Azimio la UN la kuangamiza hali zote za ubaguzi dhidi ya wanawake lililoidhinishwa na nchi 180 lilisaidia kukuza haki za wanawake kote ulimwenguni.

18. KUTOA MAJI SAFI YA KUNYWA

Wakati wa shughuli za UN za karne ya kwanza kuhusu maji (1981-1990), zaidi ya watu bilioni waliweza kupata maji kwa mara ya kwanza maishani mwao. Zaidi ya watu bilioni 1.1 walipata maji safi ya kunywa kati ya mwaka wa 1990-2002. umuhimu wa rasilimali hii ya thamani ulianza kujulikana mwaka wa 2003 ambao ni mwaka wa Maji Safi Ulimwenguni. Mwaka wa pili wa karne ya maji ulimwenguni mwaka wa (2005-2015) una lengo la kupunguza idadi ya watu wanaokosa maji safi kwa nusu.

19. KUANGAMIZA POLIO

UGONJWA WA Polio umeangamizwa katika nchi zote isipokuwa Afghanistan, Misri, India, Niger, Nigeria na Pakistan kupitia kwa mpango wa Ulimwengu wa kuangamiza Polio, juhudi kubwa zaidi Ulimwenguni za afya watu wote. Ni shukrani kwa mpango huu uliongozwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), UNICEF, Klabu cha Rotary Ulimwenguni na Kituo cha Marekani cha kudhibiti na kuzuia magonjwa, watoto takriban milioni 5 wanatembea kinyume na hapo mbeleni ambapo wangalikuwa wamepooza kwa Polio. Ugonjwa huu ulikuwa umelemaza watoto katika nchi 125 kote duniani sasa unakaribia kuangamizwa.

20. JIBU KWA UGONJWA WA UKIMWI

Shirika la Umoja wa Mataifa HIV/AIDS (UNAIDS) lililo na mipango ua kukumbwa na UKIMWI hushirikisha shughuli za dhidi ya magonjwa ya mlipuko yanayoathiri takriban watu milioni 40. shirika hili hufanya kazi katika nchi zaidi ya 130 kwa kutoa ushauri wa kuzuia UKIMWI na huduma ya matibabu, pia kupunguza idadi ya watu binafsi na jamii kuathiriwa na kuondoa athari za ugonjwa huu. UNAIDS huleta pamoja ubingwa wa mashirika 10 yanayothaminiwa na Umoja wa Mataifa

21. KUANGAMIZA NDUI

Juhudi za Shirika la Afya Ulimwenguni za miaka 13 zimesaidia kuangamiza ugonjwa wa ndui Ulimwenguni tangu mwaka wa 1980. kuangamizwa huku kumeokoa takriban dola bilioni $1 kwa mwaka ambazo zingetumiwa kwa chanjo na usimamizi, hii ni karibu mara tatu ya jumla ya gharama ya kuangamiza baa lenyewe.

22. KUTETEA KWA CHANJO ULIMWENGUNI

Kuchanja kumeokoa maisha ya watu wapatao milioni 20 na zaidi katika miongo miwili iliyo pita. Matokeo ya juhudi za UNICEF na Shirika la Afya Ulimwenguni ni kuongezeka kwa chanjo za magonjwa sita makuu yanayoweza kuzuiwa yaani Polio, Pepopunda, Surua, Kifaduro, Dondakoo na Kifua Kikuu kwa asilimia tano (5%) mwanzoni mwa mwaka wa 1970 hadi asilimia sabini na sita (76%) hivi leo. Vifo kutokana na surua vilipungua kwa karibu asilimia hamsini 50% mwaka wa 1999 hadi 2005. chanjo dhidi ya Pepopunda ziliokoa mamia ya maelfu ya kina mamama na watoto wao wachanja na nchi 104 zimeangamiza ugonjwa huo kabisa.

23. KUPAMBANA NA MAGONJWA YANAYONYONYA

Mpango wa Shirika la Afya Ulimwenguni katika nchi 11 za Afrika Magharibi kuangamiza kabisa ugonjwa wa kupofuka macho unaosababishwa na kuweza kuzuia upofu kwa watoto milioni 11 na kuanzisha kilimo katika eneo la ardhi yenye rotuba ya ukubwa wa hekta milioni 25. juhudi za wakala wa UN Afrika Kaskazini mwaka wa 1991 zilisaidia kuangamiza aina ya minyoo (screwworm) inayonyonya nyama kutoka kwa binadamu na samaki. Mipango mingine imesaidia kuokoa maisha ya wengi kutokana na minyoo (guinea worm) na magonjwa mengine ya tropiki.

24. KUKOMESHA UNEZAJI WA MAGONJWA YANAYONYONYA

Shirika la Afya Ulimwenguni lilisaidia kukomesha uenezaji wa ugonjwa mbaya uanaothiri mapafu (SARS). Kabla uangamize maelfu ya watu kwa kufuata maagiza na tahadhari kutoka kwa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na ushauri wa usafiri wa dharura uliotolewa Machi 2003, karibu nchi zote zilizokuwa na visa vya kigeni ziliweza kuzuia uenezaji au kudhibiti idadi ya visa kutoongezeka. WHO imefanya uchunguzi wa visa 200 hadi 250 vya ugonjwa wa SARS kila mwaka. Kwa kadri, Milipuko ya ugonjwa huu 5 hadi 15 inayotokea kila mwaka huhitaji mwito wa Ulimwengu mzima.

25. KUPUNGUZA VIFO VYA WATOTO

Mwanzoni mwa miaka ya 1960, motto kati ya watano aliaga dunia kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano. Kwa kutumia matibabu ya chumvi maji, udhibiti afya na kuzingatia kanuni ya lishe bora kama mawakala wa UN walivyohimiza idadi ya vifo vya watoto katika nchi zinazoendelea ilipungua kwa kiasi cha mmoja kati ya kumi na mbili ilipofika mwaka wa 2002. Lengo sasa ni kupunguza idadi ile ya 1990 ya watoto waliokufa wakiwa chini ya umri wa miaka mitano kwa thuluthi moja ifikapo 2015.

26. KUWEKA MSINGI TAYARI KWA KAZI

UN ni hodari kwa kazi. Imetoa muundo msingi wa kadri kwa uchuni wa Ulimwengu kwa kujadiliana na kukubali hali tawakwimu ulimwenguni, sheria za kiabaiashara utaratibu wa forodha, umiliki wa rasilimali, mawasiliano ya redio, television na usafiri wa meli, kushughulika shughuli zote za kutega uchumi na gharama yake. Imeweka muundo msingi tayari kwa kutega uchumi katika nchi zinazoendelea kwa kukuza utulivu wa siasa na uongozi mwema, kupambana na ufisadi na kuwa na sera imara za uchuni pia sheria njema za kibiashara.

27. KUSAIDIA VIWANADA VYA NCHI ZINAZOENDELEA

Umoja wa Mataifa kupitia kwa shirika la UN la maendeleo ya kawaida (UNIDO) limekuwa kiungo cha kuleta pamoja muungano wa viwanda kati ya kaskazini – kusini na kusini – kusini huku ukuzaji wa ujasiriamali, kutega uchumi, usambazaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda yasiyo na gharama za juu na yanayoendeleza. UNIDO imesaidia nchi kusimamia namna ya utandawazi na kupunguza umaskini kwa njia ya utaribu maalum.

28. KUWASIDIA WAHANGA WA MAAFA

Wakati maafa ya kawaida nay ale ya dharura yanapotokea, UN hushughulika na kuandaa usaidizi kwa wahanaga. Usaidizi huu kwa binadamu huweza kutekelezwa kwa sababu ya usirikiano kutoka kwa shirika la msalaba mwekundu/mwezi mwekundu na mashirika yote makuu yanayotoa misaada na wafadhili, mawakala wa UN wanaotoa misaada ya kibinadamu. Maombi ya UN husaidia kupata mchango wa dola $ bilioni 2 kwa mwaka kwa misaada ya dharura.

29. KUPUNGUZA ATHARI ZA MAAFA YA KAWAIDA

Shirika la Ulimwengu la upimaji wa hali ya hewa (WMO) limesaidia kuokoa watu milioni kutoka kwa athari hatari za kawaida na zile zilizosababishwa na binadamu. Mifumo wao wa haraka wa kutahadharisha watu kwa kutumia chombo maalum cha kujaribia usafirishaji wa matangazo ya redio/TV na setilaiti, utaalam huu umesaidia kutoa utabiri wa kweli usiopotosha. Habari kuhusu mafuta yaliyomwagika na kemikali au kuvuja kwa silaha za kinyukila na uwezo wa kutabiri nyakati za ukame kwa muda mrefu. Uwezekano wa kugawanya msaada wa chakula kwa maeneno yaliyokubwa na ukame ifaayo pia umewezekana.

30. KUTOA MSAADA WA TSUNAMI

Kati ya masaa 24 ya mafuriko ya kimbunga cha tsunami kilichoathiri bahari ya Hindi tarehe 26 Disemba 2004, Shirika la UN la kukadiria maafa na kushirikisha timu mbalimbali za msaada lilikuwa lishafika kwa maeneo yaliyokumbwa na janaga hilo zaidi. UN ilianza kushughulika kusaadia waliookoka na kuwapelekea chakula kwa watu zaidi ya milioni 1.7 na kuwapa msaada wa makao kwa wahasiriwa zaidi ya milioni 1.1, maji safi ya kunywa kwa watu zaidi ya milioni 1 pia kutoa chanjo kwa watoto zaidi ya milioni 1.2 dhidi ya shurua. Yote haya yalifanyika katika miezi 6 ya kutoa misaada. Hatua hii ya haraka ya utoaji misaada ya kibinadamu ni dhihirisho tosha kuwa maisha ya watu yaliokolewa na kuzuia vifo zaidi baada ya maafa, magonjwa pia yalizuiwa.

31. KULINDA SAFU YA OZONI

Shirika la UN la mipango ya kuhifadhi mazingira (UNEP) na shirika la Ulimwengu la maarifa ya hewa na anga (WMO) yamekuwa mstari wa mbele kwa kuarifu watu kuhusu safu ya ozoni. Makubaliano ya mapatano ya muda ya Montreal yahsaidia kuona kwamaba serikali za dunia zimesaidia kufutilia mbali matumizi ya kemikali zinazodhuru safu ya Ozoni na kubadilisha kwa kutumia ushauri mwingine usio na hatari. Juhudi hizo zitakinga mamilioni ya watu kutokana na hatari ya kupata saratani ya ngozi inayopata mtu akijiangaza kwa nuru za jua.

32. KUJISHUGHULISHA NA MABADILIKO YA HALI YA ANGA.

Shirika la kuhifadhi mazingira la Ulimwengu (GEF) hugharamia miradi kusaidia nchi zinazoendlea kupunguza madhara yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Shirika hili lilianzishwa mwaka wa 1991 na GEF ndilo shirika linalotoa michango mikubwa ya kugharamia mipango ya mazingira ulimwenguni. Husaidia pia miradi ya kuhifadhi hitilafu za uhai, kuhifadhi safu ya Ozoni, kusafisha sehemu zenye maji ulimwenguni, kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kuangamiza sehemu zozote zenye sumu na uchafu. Tangu mwaka wa 1991, GEF imekuwa ikitoa pesa dola $ bilioni 5.7 zikwemo pesa zingine 6,000 za misaada kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na makundi ya kijamii. Dola bilioni $18.8 pia zilipatikana kutoka kwa wafadhili wengine waliojiunga na GEF kusaidia. Shirika la Umoja wa Mataifa la mipango ya maendeleo (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughlikia Mazingira (UNEP) na Benki ya Dunia ni mawakala wa GEF ya kutekeleza mipango.

33. KUTEGUA MABOMU YA KUTEGWA ARDHINI

Umoja wa Mataifa unaongoza juhudi za Ulimwengu za kutegua mabomu yanayotegwa ardhini katika nchi 30 zikiwemo Afghanistan, Angola, Bosnia na Herzegovina, Iraq, Msumbiji na Sudan. Mabomu haya bado yanaua watu na kulemaza maelfu ya watu wasio na hatia kila mwaka. UN pia inafanya kazi ya kuzuia watu wasidhurike au kuingia hatarini, kusaidia majeruhi waweze kujitegemea na vilevile kusaidia nchi zilizo na mabomu haya yaliyotegwa ardhini kuyategua.

34. KUTOA MSAADA WA CHAKULA KWA WALE WANAOHITAJI

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia mipango ya chakula na ambalo ni wakala mkubwa wa kibinadamu Ulimwenguni, hufikia kwa wastani watu milioni 90 walio na njaa katika nchi 80 kila mwaka wakiwemo wakimbizi na watu waliokimbia kwao na kukosa makao. Shirika hili huzingatia lishe bora, kutoa nafaka, maharagwe, mafuta, chumvi na mchanganyiko wa chakula kilicho na vitamini na madini muhimu kwa mwili. Shirika hili la WFP la kutoa chakula hulenga kukidhi matakwa ya wanawake na watoto hasa wale walioathiriwa na njaa. Hutoa pia miradi ya kulisha watoto shuleni kwa kuwapa chakula cha mchana cha bure au chakula cha kupeleka nyumbani kwa zaidi ya watoto wa shule milioni 17. Ghara ya chakula hicho kwa kila motto ni senti 19 za kimarekani. Shughuli za shirika hili kuhusisha upangaji mzuri teknolijia ifaayo, kupakia chakula hicho kwa punda na kupandisha kwa ndege, mfumo mtandao wa satilaiti za kuona karamba chakula kimefika mahali kilipokusudiwa kwa zaidi ya karne nne WFP imeweza kutoa msaada wa chakula cha tani milioni 78.3 kwa takriban watu bilioni 1.4 kwa nchi zilizo maskini sana Ulimwenguni, hiki ni kutega uchumi cha dola $ 33.5 bilioni.

35. KUPAMBANA NA NJAA

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia kilimo na chakula (FAO) huongoza juhudi za Ulimwengi za kuangamiza njaa FAO huhudumia nchi zinazoendelea na zile zinazoendelea hivyo kuwa kama baraza lisilopendelea lililotoa nafasi kwa mataifa kukutana kwenye sawa za kujadili makubaliano na sera za majadaliano. FAO pia husaidia nchi zinazoendelea kukuza na kutumia njia za kisasa katika kilimo, elimu misitu na uvuvi na kuona kuwa kila mtu anapata lishe bora.

36. KUZUIA UVUVI WA KUPINDUKIA

Asilimia kumi na sita 16% ya uvuvi wa samaki unaofanywa ulimwenguni ni wa kupindukia kwani unawamaliza samaki wote. Asilimia nane 8% ya aina ya samaki wameangamizwa. FAO husimamia uvuvi wa baharini na kutoa tahadhari ili kuzuia uharibifu unaofanywa wa kuvua samaki wote. Ili kutatua tatizo hili, FAO na mataifa husika yamejibidisha na kuanzisha sheria maalum juu ya uvuvi unaofaa. Sheria hizi zilikubaliwa mwaka wa 1995.

37. KUPIGA MARUFUFU KEMIKALI ZENYE SUMU

Makubaliano ya Stockholm juu ya uchafu na sumu kila mara una lengo la kumaliza kemikali zote hatari zilizoko ulimwenguni. Makubaliano haya ya mwaka wa 2001 ya UN yana lengo la kumaliza aina 12 za viuadudu na kemikali za viwandani zinazodhuru na kuua watu au kuharibu mifumo ya neva na kikingamaradhi inayosababisha magonjwa kama saratani na uharibifu wa viungo vya mwili pia kuingilia ustawi wa watoto. Makubaliano mengine ya UN na utendajikazi wake umesaidia kulinda hali ya anga, kulinda hali ya uhai kuwa tofauti, kushughlikia maswala ya hali ya anga, kulinda wanyama au mimea (spishi) inayoangamizwa, kuzuia kuweko kwa majangwa, kusafisha maeneo ya bahari na kudhibiti na kumaliza upelekaji wa taka kutoka taifa lingine hadi lingine.

38. KULINDA AFYA YA WATEJA

Ili kuona kwamba chakula kinachouzwa kwenye masoko kinafaa, Shirika la Umoja wa Mataifa linashughulikia chakula na kilimo na lile linaloshughulikia Afya pamoja na ushurikiano kutoka kwa Mataifa wanachama, wameweza kuanzisha viwango vya chakula zaidi ya 200 na mipaka ya usalama zaidi ya 3000 ya vyombo vya kutilia chakula, usafirishaji na uwekaji wake. Viwango vya kuweka vitambulisho vya maelezo ili kuona kwamba mteja hapotoshwi kamwe.

39. KUPAMBANA NA UGAIDI

UN imeweka sheria maalum za kupambana na ugaidi kote Ulimwenguni. Sheria kumi na tatu zimekubaliwa kote Ulimwenguni zikisimamiwa na UN. Hizi sheria ni pamoja na zile zinazohusu utekaji watu nyara, uteka ndege nyara, milipuko wa mabomu inayosababishwa na magaidi, ufadhili wa ugaidi na hivi majuzi, ugaidi wa kinyuklia. Nchi 63 zilikubali sheria hizo kumi mwaka wa 2005. makubaliano mengine mapana mapya dhidi ya ugaidi yanatayarishwa kamati ya UN inayohusika na maswala ya ugaidi ndiyo inayosimamia jinsi nchi zinavyotii amri na kufuata masharti yaliyoweka baada ya janga la ugaidi wa Septemba 11 (9/11) na pia kuona kuwa kuna ushirikiano dhidi ya ugaidi. Afisi hii ya mihadharati na uhalifu pamoja na ushirikiano kutoka kwa mawakala mengine ya UN yamesaidia zaidi ya nchi 100 kukuza vipawa vyao vya kupambana na ugaidi.

40. KUKUZA UWEZO WA KUZAA NA AFYA YA MAMA.

Shirika la Umoja wa Mataifa lianaloshughlikia hazina ya idadi ya watu (UNFPA) limeweza kukuza haki ya watu binafsi kufanya uamuzi wao wa kupata watoto wangapi na lini kuptia kwa mipango ya uzazi ya watu kujitolea. Mipango huu umesaidia watu kufanya uamuzi unaofaa na kuzipa jamii hasa wanawake nafasi ya kudhibiti maisha yao. Matokeo ya mpango huu ni kuona kwamba wanawake katika nchi zinazoendelea wanapata watoto wachache kwa mfano watoto sita mwaka wa 1960 hadi watatu sasa na kupunguza ongezeko la watu duniani. UNFPA ilipoanza kazi mwaka wa 1969, jamii chini ya asilimia ishirini 20% walifuata mpango wa uzazi, idadi hii sasa imeongezeka na kuwa asilimia 61%. UNFPA na wenzi wake wengi pia wamesaidia kutoa usaidizi wa watu wenye ujuzi wakati wazazi wanajifungua pia kutoa misaada ya dharura hasa utunzi kwa kina mama waja wazito na kupanua huduma ya mipango ya upangaji uzazi ili kupunguza vifo kwa akina mama.

41. KUTOA UAMUZI WA KIMAHAKAMA KATIKA MABISHANO YA ULIMWENGU.

Kwa kutoa hukumu na ushauri ufaao, korti ya haki Ulimwenguni imesaidia kusuluhisha mabishano ya Ulimwengu yanayohusisha maswala ya mipaka, uhusiano wa kibalozi, utekaji nyara, haki ya mahali pa amani na salama, haki za uchumi na mengine mengi.

42. KUBORESHA UHUSIANO WA BIASHARA ULIMWENGUNI

Shirika la Umoja wa Mataifa la biashara na maendeleo (UNCTAD) limesaidia nchi zinazoendelea kujadiliana juu ya mapatnano ya kibiashara na kushinda upendeleo wa utendaji katika biashara nje. Shirika hili limejadili juu ya makubaliano ya bidhaa ulimwenguni kuona kwamba bei ni za nafuu kwa nchi zinazoendelea, kuboresha ufanisi wa muundo msingi katika biashara na kuwasaidia kuimarisha uzalishaji wa mazao na kuunganisha ndani ya uchumi wa Ulimwengu.

43. KUKUZA UREKEBISHAJI WA UCHUMI

Benki ya Dunia na Shirika la Hazina ya mambo ya fedha Ulimwenguni zimesaidia nchi nyingi kuboresha usimamizi wao wa kiuchumi, kutia misaada ya muda kwa nchi mbalimbali ili kuzirahisishia mabaku ya mikopo wanayoweza kulipa pia hutoa mafunzo kwa maafisa wa kiserikali wanaosimamia maswala ya fedha.

44. KUKUZA UTHANITI NA UTARATIBU KATIKA BAHARI ZA ULIMWENGU.

UN imeongoza katika juhudi za kudhibiti matumizi ya bahari Ulimwenguni chini ya makubaliano ya pamoja. Mapatano ya UN mwaka wa 1982 kuhusu sheria za bahari na ambayo yamekubaliwa na takriban mataifa yote ulimwenguni hutoa kwa mara ya kwanza mfumo wa sheria wa ulimwengu kwa shughuli zote juu na ndani ya bahari. Mapatano haya huwa na sheria za uimarishaji wa maeneo ya bahari, uwekaji wa mipaka ya kimataifa ya bahari, uongozaji vyombo baharini, haki na majukumu ya maeneo ya pwani na mataifa mengine, wajibu wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya bahari, ushirikiano katika kufanya utafiti wa kisayansi kuhusu bahari pia uhifadhi na kuendeleza matumizi ya viumbe hao walioko baharini.

45. KUBORESHA USAFIRI WA ANGANI NA BAHARINI.

Mashirika ya UN yamekuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna viwango vya usalama katika usafiri wa angani na baharini. Shirika la Muungano wa Kimataifa wa safari za ndege (ICAO) limechangia kufanya safari za anga kuwa usafiri wa salama. Mwaka wa 1947, watu miloni 9 walisafiri kwa ndege, 590 waliaga dunia kupitia ajali za ndege; mwaka wa 2004, idadi ya vifo ilikuwa 420 kati ya wasafiri wa ndege bilioni 3.3. isitoshe shirika la bahari Ulimwenguni (IMO) limesaidia kuona kwamba bahari ni salama. Takwimu zaonyesha kuwa usairi wa majini umeanza kuwa salama na kuboresha sifa za mazingira. Upoteaji wa meli umepungua, vifo pia vinapungua, visa vya uchafuzi pia vinapungua, uchafuzi kutokana na mafuta pia unapungua pia. Ule wa anga na maji machafu unashughulikiwa wakati huu wote kumekuwa pia na ongezeko la bidhaa zinazosafishwa baharini.

46. KUPAMBANA NA MADAWA HARAMU

Ofisi ya UN inayopambana na madawa na uhalifu imefanya kazi ya kupunguza ugavi na mahitaji ya madawa haramu kulingana na maazimio au makubaliano matatu ya UN kuhusu kudhibiti madawa na pia kushughulikia maswala ya kijamii na yale ya kiafya yanayosababishwa na utumizi mbaya wa madawa, pia madawa yanayochangia kusambazwa kwa UKIMWI. Shirika hili hufanya kazi kwa kusaidiana na mawakala wa kutekeleza sheria na kusaidia mipango ya vikundi ya jamii vinavyoshughulika kuzuia na kutibu matumizi mbaya ya madawa. Mifumo iliyowasaidia wakulima kupunguza utegemezi wa mimea haramu pia ilitolewa ili kuwasidia kuwaongoza upande wa maisha ya haki nay a kuendeleza.

47. KUPAMBANA NA UHALIFU UKLIMWENGUNI.

Ofisi ya madawa na uhalifu hufanaya kazi na nchi pia mashirika mengine ili kupambana na uhalifu wa kimataifa ukiwemo msaada wa kisheria na kiteknolojia ili kupambane na ufisadi, ubadilishanaji wa fedha, biashara haramu ya madawa ya kulevya, biashara haramu ya watu na kuingiza wakimbizi kimagendo katika nchi husika pia kuimarisha mifumo ya haki. Ofisi imesaidia kustawisha na sheria mwafaka za kilimwengu na kuona kuwa zimekubaliwa.

48. KUKUZA KAZI ZENYE HESHIMA

Shirika la wafanyikazi Ulimwenguni (ILO) limependekeza sheria na kanuni za msingi kazini zikiwemo uhuru wa kushirikiana na haki ya kujadiliana juu ya malipo, uangamizaji wa hali zote za kazi za lazima, kupiga marufuku kuajiri watoto na kuangamiza ubaguzi kazini. Shighuli muhimu za ILO ni pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi, ulinzi wa kijamii kwa wote na kuimarisha majadiliano kati ya waajiri na wafanyakazi na mashirika yao na serikali.

49. KUBORESHA ELIMU NA KUJUA KUSOMA NA KUANDIKA KATIKA NCHI ZINAZOENDELEA

Asilimia nne 4% ya watu wazima katika nchi zinazoendelea wanaweza kusoma na kuandika na asilimia 78% ya watoto huhudhuria masomo ya shule ya msingi. Lengo ni kuona kwamba watoto wote wamemaliza na kuhitimu katika shule za misingi ifikapo mwaka wa 2015. mipango iliyonuiwa kukuza elimu na maendeleo kwa wanawake ilisaidia kuongeza idadi ya wanawake waliojua kusoma na kuandika katika nchi zinazoendelea kutoka asilimia 36% mwaka wa 1970 hadi asilimia 70% mwaka wa 2000. lengo kuu ni kuona kwamba wasichana wote waweze kuhitimu katika shule za msingi na pia zile za sekondari ifikapo 2015.

50. KUPATA AHADI ZA KUSAIDIA WATOTO KOTE ULIMWENGUNI.

Kutoka El Salvador hadi Lebanon na kutoka Sudan hadi Yugoslavia, UNICEF imeongoza katika kuanzisha “siku za utulivu” na kufungua “ushoroba (njia) ya amani” ili kutoa chanjo na misaada mingine inayohitajiwa sana na watoto waliojipata katika vita. Mapatano ya Haki za Watoto yamekuwa sheria katika nchi 192. kufuatia kikao spesheli cha UN kuhusu watoto, serikali 192 zilijitolea kwa kufuata kanuni katika nyanja za afya, Elimu, ulinzi dhidi ya maonevu, unyonyaji na vurugu na mapambano dhidi ya UKIMWI.

51. KUHIFADHI MAENEO YA HISTORIA KIJAMII NA MAJENGO YALIYOSANIFIWA.

UNESCO imesaidia nchi 81 kuhifadhi majengo ya kumbukumbu na mapatano ya kilimwengu yamekubaliwa ili kusaidia kulinda rasilimali za kitamaduni.

52. KURAHIHISHA MABADILISHANO YA KIJAMII NA KITAALUMA.

Shirika la Umoja wa Mataifa kupitia UNESCO na Chuo Kikuu cha Umoja wa Mataifa yamehimiza usirikiano wa litaalamu na kisayansi kuhusisha mifumo mbalimbali ya Taasisi na kukuza tamaduni zote hata zile za watu walio wachache na wa asili.

53. KULINDA RASILIMALI ZA WASOMI

Shirika la Mali ya Wasomi Ulimwenguni (WIPO) hulinda haki za wasanii na wanaomiliki rasilimali za wasomi kote ulimwenguni na kuona kwamba wavumbuzi na waandishi wanajulikana na kupewa tuzo kwa ubunifu wao. Ulinzi wa haki za wasomi huwa kama kichocheo cha ubunifu wa binadamu, kusukuma mbele mipaka ya sayansi na ufundi, kuimarisha dunia ya fasihi na usanii. Kwa kuandaa mazingira yafaayo kwa uuzaji wa bidhaa za rasilimali za wasomi, magurudumu ya biashara ya Ulimwengu yatakuwa yametiwa mafuta.

54. KUKUZA UHURU WA MAGAZETI NA ULE WA KUJIELEZA.

Ili kuwaruhusu watu wote waweze kuoata habari ambazo hazitakaguliwa na kutokuwa na ubaguzi wa kitamaduni na kutokuwa na ubaguzi wa kitamaduni, UNESCO imesaidia kustawisha na kuimarisha vyombo vya habari, imesaidia kuanzisha mawakala huru wa habari na kusaidia uhuru wa magazeti. UNESCO pia inahudumu kama shirika la kulinda uhuru wa magazeti, kushutumu waziwazi ukiukaji wa sheria kama mauaji na waandishi wa magazeti kutiwa kizuizini.

55. KUBADILISHA MITAA YA MABANDA IWE MAKAO YAFAAYO KWA BINADAMU.

Miji mikuu imekuwa makao kwa nusu ya watu ulimwenguni. Wamekuwa kitovu cha shughuli za uzalishaji mali na kutumia. Pia hushughulikia namna za kutega uchumi na uimarishaji wa jamii ili kupata mali na nafasi bora. Miji mikuu mingi hasa katika nchi zinazoendelea, wakazi wa mitaa ya mabanda ni zaidi ya asilimia 50% ya watu wote na wengi wao wana makao haba au hawana kabisa, pia ukosefu wa maji na udhibiti afya. Shirika la UN la makao ulimwenguni yaani HABITAT lililo na miradi na mipango ya ufundi zaidi ya 150 katika nchi 61 kote duniani, hushirikiana na serikali, serikali za mitaa na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuvumbua na kutatua matatizo ya miji na miji mikuu. Hutoa usalama wa unilikaji kwa wale wakazi waskini wa mjini, jambo hili huwa kama kichocheo cha rasilimali kwa huduma za kimsingi na nyumba kwa watu maskini.

56. KUKUZA HUDUMA ZA POSTA ULIMWENGUNI

Muungana wa Posta ulimwenguni (UPU) ni Baraza muhimu kwa ushirikiano wa huduma za Posta ulimwenguni, pia husaidia kuona kwamba mfumo wa kweli wa kilimwengu unaboresha bidhaa na huduma zake. Huweka sheria za ubadilishaji wa barua ulimwenguni na kupendekeza maendeleo ya uzalishaji bidhaa kama barua na kuboresha kiwango cha huduma kwa wateja wake. Huduma za UPU zina wanachama wan chi 190 na kuunda mfumo mkubwa wa usambazaji katika ulimwengu, usafirishaji wa bidhaa za barua bilioni 430 kila mwaka.

57. KUANZISHA KILIMO CHA KISASA NA KUPUNGUZA GHARAMA

Kupitia msaada kutoka kwa Shirika la chakula na kilimo, mazao, sera na mifumo imeimarika pia kushiriki kwa wenyeji. Wakulima wa mchele kutoka Asia wamefaidi kwa kuokoa zaidi ya dola milioni $50 kwa mwaka kutokana na gharama ya viuadudu huku serikali ikifaidi kwa kuokoa zaidi ya dola $150 milioni kwa mwaka kupitia kwa misaada ya viuadudu ambayo ingetumiwa. Manufaa katika mazingira na afya yaliyopatikana kutokana na upunguzaji wa matumizi ya viuadudu umekadiriwa kuwa zaidi ya dola $10 milioni kwa mwaka.

58. KUKUZA HAKI ZA WALEMAVU

Umoja wa Mataifa umekuwa katika mstari wa mbele ukipigania usawa kamili wa watu walio na ulemavu, kukuza kushiriki kwao kwa mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. UN imeonyesha kuwa watu walio na ulemavu ni muhimu kwa jamii na sheria za kwanza kabisa za kutetea haki zao na hadhi yao kote duniani zinaandikwa.

59. KUBORESHA HALI MBAYA YA WENYEJI

Umoja wa Mataifa umefichua udhalimu dhidi ya watu wa asili au wenyeji 370 milioni wanaoishi katika nchi 70 kote ulimwenguni. Watu haawa ni baadhi ya wale walio na hitilafu na wale wanaoweza kudhuriwa kote duniani. Wanachoma 16 wa kudumu katika Baraza la maswala ya kiasili lililoanzishwa mwaka wa 2000 hufanya kazi ili kuboresha hali ya watu wa asili kote ulimwenguni katika maendeleo, utamaduni, Haki za kibinadamu, mazingira, Elimu na Afya.

60 KUBORESHA HALI YA WATU WA ASILI

Umoja wa Mataifa umefichua dhuhima wanazofanyiwa watu wa asili milioni 370 wanaoishi katika nchi 70 kote ilimwenguni na ni watu walioathiriwa na hali ngumu hasa umaskini. Kamati ya wanachama wa kudumu 16, wanoshughulikia maswala ya watu wa asili ilianzishwa mwaka wa 2000 na hufanya juhudi za kuboresha na kuinua hali ya maisha ya watu wa asili kote ulimwenguni katika maendeleo, tamaduni, haki za kibinadamu, mazingira, elimu na afya.

KWA MAELEZO ZAIDI, juu ya malengo ya Ustawi wa Milenia tazama

www.un.org/ milleniumgoals
www.milleniumcampaign.org
http:// milleniumindicators.org

SIFA ZA PICHA

Ukurasa 2 Jorgen Schytte/ Picha za kawaida;
Ukurasa 5 Picha ya UN/ Martine Perret
Ukurasa 6 Picha ya UN/ Martine Perret; Ukurasa wa 8 Luiz C. Marigo/ Picha za kawaida; Ukurasa wa 11 Timothy Clary; Ukurasa wa 13 Picha ya UN/ R. Chalasani; Ukurasa wa 14 Picha ya UN/ Stephenie Hollyman, Ukurasa wa 17 Picha ya UN Ky Chung; Ukurasa wa 18 Hlaing Thntint; Ukurasa wa 20 Ron Giling/ Picha za kawaida Ukurasa wa 21 Shehzad Noorani/ Picha za kawaida; Ukurasa wa 22 kitabu cha MDG, Ukurasa wa 24 Picha ya UN; Ukurasa wa 27 Picha ya UN/ Jorge Aramburu; Ukurasa wa 29 WFP, Ukurasa wa 32 Sean Sprague picha za kawaida; Ukurasa wa 34 Macduff Everton/ Benki ya picha; Ukurasa wa 35 Dougal Waters/ Diski ya Picha nyekundu; Ukurasa wa 37 Magnum/ Steve McCurry; Ukurasa wa 39 Picha ya UN; Ukurasa wa 40 Peter Schikert/ Picha ya kawaida; Frans Lemmens/ Picha za Kawaida, Chlaus Lotscher/ Picha za kawaida, Otto Stadler/ Das Fotoarchiv; Ukurasa wa 41 Ron Giling/ Picha za Kawaida, Chlaus Lotscher/ Picha za kawaida,Otto Stadler/ Das Fotoarchiv; Ukurasa wa 43 Panos/ Mark Henley; Ukurasa wa 44 WFP; Ukurasa wa 47 Luis Delgado Hurtado; Ukurasa wa 48 TELECOM.

Kimetayarishwa na Umoja wa Mataifa, Idara ya Habari kwa Umma -53269-OKTOBA 2005-IOM.